45. Marekebiso ya kifungu cha 35B.
46. Marekebiso ya kifungu cha 64.

*(c) Marekebiso ya Sheria ya Usimamizi wa Kumbukumbu,  
Sura ya 309*

47. Tafsiri.
48. Marekebiso ya kifungu cha 2.

*(d) Marekebiso ya Sheria ya Benki na Taasisi za Kifedha,  
Usimamizi wa , Sura ya 342*

49. Tafsiri.
50. Marekebiso ya kifungu cha 8.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



**NA.13 YA 2015**

**NAKUBALI,**

**JAKAYA MRISHO KIKWETE,**

*Rais*

*25 Aprili, 2015*

**Sheria kwa ajili ya kuweka utambuzi wa kisheria wa miamala ya kielektroniki, huduma za Serikali mtandao, matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika ukusanyaji wa ushahidi, kukubalika kwa ushahidi wa kielektroniki; urahisishaji wa matumizi ya saini salama za kielektroniki na mambo mengine yanayohusiana na hayo.**

**IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

**SEHEMU YA KWANZA  
MASHARTI YA UTANGULIZI**

Jina na tarehe  
ya kuanza  
kutumika

- 1.** Sheria hii itaitwa Sheria ya Miamala ya Kielektroniki ya mwaka 2015 na itaanza kutumika kwa tarehe ambayo Waziri, kwa Tangazo litakalo chapishwa kwenye *Gazeti la Serikali*, atateua.

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-  
 “kuingia” kuhusiana na mfumo wowote wa kompyuta maana yake ni kupata fursa ya kuingia, kutoa kuelekeza, kuwasiliana na, kuhifadhi data katika, kupokea data kutoka katika au vinginevyo kutumia rasilimali zozote za mfumo wa kompyuta au mtandao au mfumo wa kifaa cha kutunzia data ;  
 “mlengwa” maana yake ni mtu au mhusikaambaye amedhaminiwa na mtumaji taarifa kupokea mawasiliano ya kielektroniki, isipokuwa haitajumuisha mtu anayetenda kama mtu kati kuhusiana na mawasiliano ya kielektroniki;  
 “mfumo wa kompyuta” maana yake ni kifaa au mjumuiko wa vifaa, ikijumuisha mtandao, vifaa vya kwingiza na kutoa vinavyoweza kutumika pamoja na majalada ya nje ambayo yana programu za kompyuta, maelezo yakielektroniki, data zinazoingia na zinazotoka ambazo zinaleta mantiki, uhifadhi wa data za namba na udhibiti wa mawasiliano yanayorejea;  
 “mtumiaji” maana yake ni mtu yejote ambaye anayeingia au anayekusudia kuingia katika muamala wa kielektroniki na mtoa huduma akiwa kama mtumiaji wa mwisho wa bidhaa au huduma zinazotolewa na mtoa huduma;  
 “kriptografia” maana yake ni utaalim wa kulinda taarifa kwa kuzibadilisha kuwa kwenye mfumo usiosomeka;  
 “data” maana yake ni taarifa yoyote iliyowasilishwa kwa njia ya kielektroniki;  
 “ujumbe wa data” maana yake ni ujumbe uliyotengenezwa, uliyowasilishwa, uliyopokelewa au kutunzwa kwa

njia ya kielektroniki, kwa simaku au njia nyingine yoyote katika mfumo wa mawasiliano au kwa ajili ya kusafirishwa kutoka katika mfumo mmoja wa mawasiliano

kwenda kwenye mfumo mwengine;  
“mawasiliano ya kielektroniki” manta yake ni uhamishaji  
wowote wa alama, mawimbi au data zozote za  
kompyuta za aina yoyote zilizosafirishwa kwa  
mkupuo au sehemu kwa njia ya waya, redio,  
sumaku, picha za kielektroniki, picha za kioo au kwa  
njia nyingine yoyote zinazofanana na hiyo;  
“Gazeti la Serikali la kielektroniki” maana yake ni Gazeti la  
Serikali linalorejewa kwenye kifungu cha 16;  
“kumbukumbu ya kielektroniki” maana yake ni  
kumbukumbu iliyotunzwa kwa njia ya kielektroniki;  
“saini ya kielektroniki” maana yake ni data, ikijumuisha,  
sauti ya kielektroniki, alama au mchakato  
uliofanyika au kutumika katika kumtambua  
mhusika, ili kuashiria ridhaa au kusudio lake  
kuhusiana na taarifa iliyoko katika mawasiliano ya  
kielektroniki na ambayo imeambatanishwa kwenye  
au kimantiki inahusiana na mawasilano ya  
kielektroniki;  
“muamala wa kielektroniki” maana yake ni muamala,  
kitendo au fungo la miamala ama ya kibiashara au  
yasiyo ya kibiashara ambayo inafanyika kwa njia  
ya kielektroniki;  
“mfumo wa ujumbe unaojiendesha” maana yake ni mfumo  
unaojiendesha wenyewe au programu nyingine

iliyoandaliwa awali, inayotumika kuanzishia kitendo, kujibu mawasiliano ya kielektroniki au kuzalisha kazi nyingine kwa ukamilifu au kwa sehemu pasipo kurejea au kuingiliwa na mhusika kila wakati kitendo kinapofanywa au jibu linapotolewa na mfumo;

“Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano;

“mtuma taarifa” maana yake ni mtu ambaye kutoka kwake mawasiliano ya kielektroniki yanadaiwa kuwa aliyatuma au kuyayazalisha;

“sehemu ya biashara” maana yake ni sehemu yoyote ambayo mhusika anatunza ana mahala pa kuendesha shughuli ya kiuchumi mbali ya shughuli ya muda ya uuazaji wa bidhaa au huduma katika eneo maalum.

#### **SEHEMU YA PILI UTAMBUZI NA MATOKEO YA MIAMALA YA KIELEKTRONIKI**

Kutambulika  
kwa ujumbe  
wa data

Uhalali wa  
muamala wa  
kielektroniki

**4.** Ujumbe wa data hautakataliwa nguvu ya kisheria, uhalali au ktumuika kwake kwa sababu ya kuwa umetengenezwa katika mfumo wa kielektroniki.

**5.-(1)** Endapo sheria inahitaji taarifa au muamala kuwa katika namna iliyoainishwa isiyo ya kielektroniki au kimaandishi, masharti hayo yatakuwa yametimizwa na taarifa au muamala wa kielektroniki ambayo-

- (a) imewekwa katika namna sawa au inayokaribiana na namna maalum isiyo ya kielektroniki;
- (b) inaweza kufikiwa na mtu mwengine kwa ajili ya rejea; na

(c) ina uwezo wa kuhifadhiwa na mtu huyo mwingine.

(2) Kifungu kidogo cha (2) kitatumika iwapo maelekezo ya kuwa katika maandishi ni ya lazima au iwapo sheria inaainisha madhara ya taarifa ambayo haiko kimaandishi.

Saini ya  
kielektroniki

**6.-**(1) Endapo sheria inahitaji saini ya mtu, kuwekwa masharti hayo yatatimizwa kwa kuweka salama na saini ya kielektroniki iliyowekwa chini ya Sheria hii.

(2) Masharti yanayohitaji saini ya kielektroniki chini ya kifungu kidogo cha (1) yatakuwa yametimizwa iwapo:

(a) njia hiyo inatumika kumtambua huyo mtu na kuonesha nia ya mtu huyo kuhusu taarifa iliwasilishwa;

(b) wakati wa matumizi ya njia hiyo, njia hiyo ilikuwa inaaminika na sahihi kwa madhumuni ambayo taarifa ilimesilishwa.

(3) Wahusika katika mkataba wanaweza kukubaliana kutumia njia fulani ya kusiani ya kielektroniki kwa kadri watakavyoona inafaa, isipokuwa kama imeelezewa vinginevyo na sheria.

Saini salama  
ya  
kielektroniki

**7.** Saini ya kielektroniki itachukuliwa kuwa ni salama iwapo:

(a) ni ya kipekee kwa madhumuni ambayo inatumika;

(b) inaweza kutumika kumtambua mtu ambaye anasaini mawasiliano ya kielektroniki;

(c) inatengenezwa na kuwekwa kwenye mfumo wa mawasiliano ya kielektroniki na mweka saini;

(d) ipo chini ya udhibiti wa mweka saini; na

(e) imetengenezwa na kuunganishwa kwenye mawasiliano ya kielektroniki ambayo inahusiana nayo kwa namna ambayo iwapo kuna mabadiliko yoyote yanafanyika kwenye mawasiliano ya kielektroniki, mabadiliko hayo yatafichuliwa.

Matumizi ya  
saini salama  
ya  
kielektroniki

Kutunza  
kumbuku-  
mbu  
kielektroniki

- 8.** Saini salama ya kielektroniki itachukuliwa kuwa imetumika iwapo:
- (a) imetumwa na mmiliki wa saini salama ya kielektroniki;
  - (b) inawekwa na mmiliki kwa lengo la kusaini au kuthibitisha mawasiliano hayo ya kielektroniki.

**9.-(1)** Endapo sheria inahitaji taarifa fulani au nyaraka kutunzwa, masharti hayo yatakuwa yametimizwa kwa kutumia taarifa ya kielektroniki, ilimradi masharti yafuatayo yatazingatiwa:

- (a) taarifa iliyomo kwenye kumbukumbu hiyo ipo katika njia ya kielektroniki,
- (b) kumbukumbu ya kielektroniki inashikiliwa au kuwekwa katika namna ambayo imezalishwa, imetumwa au imepokelewa au ipo katika mpangilio ambao umewekwa wazi ili kuonyesha taarifa hiyo ni saini; na
- (c) taarifa hiyo ya kielektroniki inashikiliwa au inatunzwa katika namna ambayo inawezesha utambuzi wa chanzo na sehemu ambayo taarifa hiyo ya kielektroniki au mawasiliano ya kielektroniki yanaelekea na tarehe na muda ambao ilitengenezwa au ilizalishwa, ilitumwa, ilipokelewa au kutunzwa.

(2) Wajibu wa kushikilia au kutunza nyaraka, kumbukumbu au taarifa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) hautahusu taarifa yoyote ambayo madhumuni yake pekeeni ni kuwezesha ujumbe kutumwa au kupokelewa.

Uthibitisho

**10.** Endapo sheria inahitaji-

- (a) saini, maelezo au nyaraka kuthibitishwa, rasmi, kukubaliwa, kuidhinishwa au kutolewa chini ya kiapo, masharti hayo yatachukuliwa kuwa yametimizwa iwapo saini ya kielektroniki ya mtu aliyeidhinishwa kutekeleza wajibu huo imeambatanishwa, imejumuishwa au katika hali ya kawaida inahusishwa na saini ya kielektroniki au ujumbe wa data;
- (b) mtu kutoa nakala ya nyaraka iliyoidhinishwa rasmi na nyaraka hiyo ipo katika mfumo wa kielektroniki, masharti hayo yatakuwa yametimizwa iwapo mtu huyo atatoa nakala ya nyaraka iliyochapishwa na kuthibitishwa.

Masharti  
mengineyo**11.-(1)** Endapo Sheria inahitaji-

- (a) kuwasilishwa kwa nakala zaidi ya moja ya nyaraka kwenda kwa mlengwa mmoja kwa wakati mmoja, masharti hayo yatakuwa yametimizwa kwa uwasilishaji wa wasiliano moja la kielektroniki ambalo lina uweza wa kutolewa nakala na mlengwa huyo;
- (b) lakiri na saini kuwekwa kwenye nyaraka na sheria hiyo haiweki utaratibu au namna ambavyo nyaraka hiyo inaweza kufungwa au kuwekewa lakiri kwa njia ya kielektroniki, masharti hayo yatakuwa yametimizwa iwapo nyaraka hiyo itafungwa na kuwekewa lakiri na kusainiwa kwa njia ya kielektroniki na mtu ambaye alitakiwa kusaini na kuweka lakiri nyaraka hiyo;
- (c) mtu kutuma taarifa au nyaraka kwa njia ya posta au huduma sawa na hiyo, masharti hayo yatakuwa

yametimizwa iwapo taarifa au nyaraka **hiyo** imetumwa kwa njia ya kielektroniki.

(2) Maneno yaliyomo kwenye sheria, ikijumuisha maneno “nyaraka”, “kumbukumbu”, “jalada”, “wasilisha”, “peleka”, “fikisha”, “chapisha”, “andika kwenye” au maneno au matamshi yenyе maana kama hayo, yatatafsiriwa kwa namna ambayo itaruhusu aina, mfumo au tendo hilo kuwiana na mawasiliano ya kielektroniki isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo chini ya Sheria hii.

Mwenendo  
wa mtu  
anayetumia  
saini ya  
kielektroniki

**12.** Mtu anayetumia saini ya kielektroniki atawajibika kisheria kwa kushindwa kuchukua hatua stahiki kuthibitisha-

- (a) kuhakikisha uhalali wa saini inayotumika; na
- (b) uhalali wa cheti au kuzingatia masharti yanayo husiana na cheti iwapo saini ya kielektroniki inawiana na cheti.

#### SEHEMU YA TATU HUDUMA ZA SERIKALI MTANDAO

Utambuzi wa  
huduma za  
Serikali  
mitandao

**13.-**(1) Bila ya kuathiri sheria nyingine yoyote, ambapo taasisi ya umma ina mamlaka ya kushughulikia taarifa au nyaraka au kutoa huduma, inaweza kushughulikia taarifa au nyaraka hiyo au kutoa huduma hizo kwa njia ya kielektroniki kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Masharti kuwa taarifa au nyaraka itatolewa kimaandishi au kusainiwa haitatafsiriwa kuzuia matumizi ya njia ya kielektroniki.

(3) Taasisi ya umma inaweza kuchukua au kupokea malipo kwa njia ya kielektroniki kwa namna itakavyoainishwa.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Serikali Mtandao na kwa Tangazo litakalo chapishwa kwenye *Gazeti la Serikali*, kutoa miongozo itakayo ainisha-

- (a) namna na mfumo ambao muamala wa kielektroniki unaweza kufanyika;
- (b) aina ya saini ya kielektroniki inayohitajika, pale ambapo muamala wa kielektroniki unatakiwa kusainiwa;
- (c) namna na mfumo ambao saini ya kielektroniki inaweza kuambatanishwa au kuhusishwa na muamala wa kielektroniki;
- (d) mchakato wa udhibiti na taratibu za kuhakikisha uadilifu usalama na usiri wa taarifa;
- (e) utambulisho au utaratibu utakaozingatiwa na mtoa huduma aliyeidhinishwa kwa ajili ya kuwasilisha muamala wa kielektroniki;
- (f) mchakato wa udhibiti na utaratibu utakao hakikisha uadilifu wa kutosha, usalama na usiri wa muamala wa kielektroniki au malipo yakielektroniki; na
- (g) masharti mengine kwa yoyote ambayo yanahusiana na miamala ya kielektroniki.

(5) Bila kujali kifungu kidogo cha (4), taasisi yoyote iliyoidhinishwa, inaweza kutumia taratibu nyingine za uthibitishaji.

Uwasilishaji  
wa nyaraka  
kwa njia ya  
kielektroniki

**14.-**(1) Endapo sheria inahitaji nyaraka kuwasilishwa, masharti hayo yatakuwa yametimizwa iwapo nyaraka hiyo imewasilishwa kwa njia ya kielektroniki.

(2) Kifungu kidogo cha (1) kitatumika pale ambapo kuna mfumo wa kuandaa taarifa ambao unaweza-

- (a) kutambua chanzo, mwelekeo, muda na tarehe ya kutowasilishwa, kutuma na kupokea kwa taarifa;
- (b) kuthibitisha kupokewa kwa nyaraka.

Malipo ya fedha na utoaji wa stakabadhi kwa njia ya kielektroniki

**15. Endapo sheria inahitaji-**

- (a) malipo kufanyika, masharti hayo yatakuwa yametekelizwa iwapo malipo yatakuwa yamefanyika kwa njia ya kielektroniki na kukidhi masharti yoyote yaliyotolewa na sheria nyininge husika; na
- (b) utoaji wa stakabadhi yoyote ya malipo, masharti hayo yatakuwa yametekelizwa iwapo stakabadhi hiyo itakuwa katika mfumo wa ujumbe wa kielektroniki na ujumbe kusomeka na unaeleweka kiasi kwamba unaweza kutumika katika rejea.

Uchapishaji wa nyaraka

**16. Endapo sheria inahitaji nyaraka kuchapishwa kwenye *Gazeti la Serikali*, masharti hayo yatakuwa yametimizwa iwapo nyaraka hiyo itachapishwa kwenye *Gazeti la Serikali* la kielektroniki.**

Nyaraka katika mfumo wa kielektroniki haitakuwa lazima

**17. Sheria hii haitatoa haki kwa mtu ye yoyote kushinikiza taasisi ya yoyote ya umma kushughulikia nyaraka yoyote kielektroniki.**

#### SEHEMU YA NNE

#### KUKUBALIKA NA UZITO WA USHAHIDI WA UJUMBE WA DATA

Kukubalika kwa ujumbe wa data

**18.-(1) Katika mwenendo wa shauri lolote la kisheria, kanuni za ushahidi kitakacho tumika ili kukataa kukubalika kwa ushahidi wa ujumbe data kwa kigezo kwamba ni ujumbe data.**

(2) Katika kuamua kukubalika na uzito wa ushahidi wa ujumbe data, yafuatayo yatazingatiwa-

- (a) kuaminika kwa namna ambayo ujumbe data umetengenezwa, umehifadhiwa au umewasilishwa;
- (b) kuaminika kwa namna ambayo uadilifu wa ujumbe data ulivyohifadhiwa;

(c) namna ambayo chanzo cha ujumbe data kimetambuliwa;

(d) vigezo vingine vyovoyote vinavyofaa katika kutathmini uzito wa ushahidi huo.

(3) Uhalali wa kumbukumbu za mfumo wa kielektroniki ambamo kumbukumbu ya kielektroniki inanukuliwa au kutunzwa, iwapo hakuna ushahidi kinyume na, utachukuliwa kuwa-

(a) iwapo kuna ushahidi unaothibitisha ukweli kuwa katika muda wote, mfumo wa kompyuta au kifaa kama hicho kilikuwa kinafanya kazi vizuri au iwapo hakikuwa kinafanya kazi vizuri, kitendo cha kutokufanya kazi kwake vizuri hakukuathiri uadilifu wa kumbukumbu ya kielelektroniki na hakuna sababu nyingine za msingi kushuku uhalali wa kumbukumbu za mfumo wa kielektroniki;

(b) iwapo inabainika kwamba kumbukumbu ya kielektroniki ilirekodiwa au kuhifadhiwa na mhusika katika shauri ambaye ana maslahi tofauti na mhusika wa upande unaotaka kuutumia ushahidi huo; au

(c) imebainika kuwa kumbukumbu ya kielektroniki ilirekodiwa au kuhifadhiwa katika utendaji kazi wa kawaida na mtu ambaye si mhusika katika shauri na ambaye hakurekodi au kuhifadhi kumbukumbu chini ya uangalizi wa mhusika wa upande unaotaka kuutumia ushahidi huo.

(4) Kwa madhumuni ya kuamua iwapo kumbukumbu ya kielektroniki inakubalika chini ya kifungu hiki, ushahidi unaweza kutolewa kuhusiana na kiwango chochote kilichowekwa, taratibu, mila au uzoefu kuhusiana na namna ambavyo

kumbukumbu za kielektroniki zinatakiwa kuchukuliwa au kunakiliwa au kutunzwa kwa kuzingatia aina ya biashara au mfumo unaotumika, au kutunza kumbukumbu ya kielektroniki na chanzo na madhumuni ya kumbukumbu ya kielektroniki.

Chanzo cha mawasiliano ya kielektroniki

**19.** Mawasiliano ya kielektroniki yatachukuliwa kuwa yametoka kwenye chanzo iwapo yametumwa na-

- (a) chanzo chenyewe;
- (b) mtu ambaye ameidhinishwa kwa namna hiyo na chanzo ili kufanya mawasiliano kwa njia ya kielektroniki kuhusiana na ujumbe data; au
- (c) mfumo wa kompyuta katika programu unaojiendesha yenyewe uliyowekwa na au kwa niaba ya chanzo.

Kuwasilisha nyaraka halisi katika mfumo wa kielektroniki

**20.-(1)** Endapo sheria inamtaka mtu kwasilisha nyaraka au taarifa, matakwa hayo yatakuwa yametimizwa iwapo-

- (a) mtu huyo anawasilisha, kwa njia ya mawasiliano ya kielektroniki katika mfumo wa kielektroniki, fomu au nyaraka hiyo;
- (b) kwa kuzingatia mazingira yote husika, wakati mawasilano hayo ya kielektroniki yanatumwa, mfumo wa kutoa taarifa ya kielektroniki ya nyaraka hiyo ultoa njia ya uhakika ya kuhakikisha utunzaji wa uadilifu wa taarifa iliyoko kwenye nyaraka;
- (c) wakati mawasiliano ya kielektroniki yanatumwa, ilikuwa ni sahihi kutarajia kuwa taarifa iliyoko ndani ya nyaraka hiyo au taarifa ingeweza kupatika na kwa urahisi ili kuiwezesha kutumika katika rejea ya taarifa hiyo.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), uadilifu wa taarifa iliyoko kwenye nyaraka utakuwa umezingatiwa iwapo taarifa itabaki kuwa kamili na hajabertilishwa, isipokuwa kwa:

- (a) kuweka nyongeza ya uthibitisho **wowote**; au
- (b) mabadiliko yoyote ya msingi, ambayo yanatokea wakati wa kufanya mawasiliano ya kawaida, utunzaji au uwekaji wazi.

**SEHEMU YA TANO  
UTAMBUZI WA MIKATABA YA KIELEKTRONIKI**

Utambuzi wa mikataba ya kielektroniki

**21.-**(1) Kwa madhumuni ya kuondoa shaka, mkataba unaweza kuandaliwa kwa njia ya kielektroniki isipokuwa kama imekubaliwa vinginevyo na wahusika.

(2) Endapo kumbukumbu za kielektroniki zinatumika katika kuandaa mkataba, mkataba huo hautapoteza nguvu ya kisheria au uwezo wa kutekelezwa kutokana na sababu kuwa kumbukumbu za kielektroniki zilitumika kwa madhumuni hayo.

Muda wa kutuma na kupokea mawasiliano ya kielektroniki

**22.-**(1) Taarifa iliyoko kwenye mfumo wa kielektroniki itachukuliwa kuwa imetumwa pale inapoingia kwenye mfumo wa mawasiliano ulio nje ya uwezo wa chanzo cha taarifa au mtu ambaye aliituma taarifa hiyo ya kielektroniki kwa niaba ya chanzo.

(2) Endapo au mlengwa wa taarifa wapo kwenye mfumo mmoja wa mawasiliano ya kielektroniki, taarifa ya kielektroniki itachukuliwa kuwaimewasilishwa pale ambapo mlengwa anaweza kupata taarifa hiyo.

(3) Endapo mlengwa ametenga mfumo wa kompyuta kwa madhumuni ya kupokea mawasiliano ya kielektroniki, taarifa hiyo itachukuliwa kuwa imepokelewa wakati mawasiliano ya kielektroniki yanaingia kwenye mfumo wa mawasiliano uliotengwa.

(4) Endapo mawasiliano ya kielektroniki yanatumwa kwenye mfumo wa mawasiliano wa mlengwa ambao ni tofauti na mfumo wa kompyutauliotengwa, taarifa hiyo itachukuliwa kuwa imewasilishwa-

- (a) wakati ambapo mawasiliano ya kielektroniki yanaweza kupokelewa na mlengwa katika anwani hiyo; na
- (b) mlengwa anajua kuwa mawasiliano ya kielektroniki yametumwa kwenye anwani hiyo.

(5) Endapo mlengwa hajatenga mfumo wa mawasiliano, upokeaji wa taarifa unatimia pale ambapo mawasiliano ya kielektroniki yanapokelewa na mlengwa, au yalitakiwa katika kikawaida yakupokelewa na mlengwa.

Uthibitishaji  
wa upokeaji  
mawasiliano

**23.-(1)** Uthibitisho wa kupokea mawasiliano ya kielektroniki, iwapo chanzo na mlengwa hawajakubaliana kuhusu namna au njia ya mawasiliano, unaweza kutolewa kwa-

- (a) njia ya kielektroniki na mlengwa, ama kwa njia ya ujumbe kujiendesha wenyewe au vinginevyo; au
- (b) kwa kuititia kitendo chochote kilichofanywa na mlengwa, ambacho kinatosha kuashiria kwa chanzo cha mawasiliano kuwa mawasiliano ya kielektroniki yamepokelewa.

(2) Endapo chanzo cha mawasiliano ameainishakuwa mawasiliano ya kielektroniki yatawabana wahusika pale tu anapopokea uthibitisho wa kupokea au unapokelewa, na uthibitisho haujapokelewa, mwanzilishi atatakiwa-

- (a) ndani ya muda uliotajwa au kukubalika au, iwapo muda haujatajwa au kukubalika, ndani ya muda wa

kawaida, basi chanzo cha mawasiliano kinaweza kutoa taarifa kwenda kwa mlengwa ikielezea kuwa hakuna uthibitisho aliyopokea na ikiainisha muda wa kawaida ambao kwayo uthibitisho wa taarifa unatakiwa kuwa umepokelewa naye; au

- (b) ndani ya ukomo wa muda uliotajwa, anaweza, baada ya kutoa taarifa kwa mlengwa, kuyachukulia mawasiliano hayo ya kielektroniki kama vile hayakuwahi kutumwa kabisa.

Mahali pa  
kutuma na  
kupokea  
mawasiliano  
ya  
kielektroniki

**24.-**(1) Isipokuwa kama imekubalika vinginevyo kati ya chanzo cha mawasiliano na mlengwa, mawasiliano ya kielektroniki yatachukuliwa kuwa yametumwa kwenye sehemu ambapo chanzo cha mawasiliano kinaendesha biashara yake na yatachukuliwa yamepokelewa katika sehemu ambayo mlengwa anaendesha biashara yake.

- (2) Kifungu kidogo cha (1) kitatumika-

- (a) hata kama chanzo cha taarifa au mlengwa hakuwepo katika sehemu yake ya kawaida ya biashara; na

- (b) kuamua sehemu ambapo mkataba uliingiwa kwa madhumuni ya kulipa kodi.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), iwapo chanzo cha mawasliano au mlengwa -

- (a) ana sehemu ya biashara zaidi ya moja, sehemu ya biashara itakuwa ni:

- (i) ile ambayo inahusiana kwa karibu zaidi na muamala husika kwa kuzingatia mazingira yanayojulikana au ya kufikiriwa na wahusika katika muda wowote kabla au wakati wa kufikia makubaliano ya mkataba; au

(ii) pale ambapo hakuna muamala, sehemu yake aliyoizoea kwa ajili ya biashara.

(4) Iwapo kampuni hodhi haina sehemu ya biashara, sehemu ya biashara itakuwa ni anwani ya kibashara ya kampuni hiyo au sehemu ilisajiliwa au kuanzishwa kisheria.

(5) Kifungu hiki kitatumika bila kujali kwamba sehemu ambapo mfumo wa kompyuta unaowiana na unawezesha kupatikana kwa anwani ya kielektroniki upo katika sehemu iliyotofauti na sehemu ambapo mawasiliano yakielektroniki yatachukuliwa kuwa yamepelekwa au kupokelewa.

Muda na mahali  
ambapo mkataba  
umefungwa

**25.-**(1) Endapo wahusika wanaingia kwenye mkataba kwa njia ya kielektroniki, mkataba huo utakuwa umefungwa kwa muda huo na sehemu ambayo mawasiliano ya makubaliano yalipokelewa.

(2) Mapendekezo ya mkataba yaliyo katika mfumo wa kielektroniki yatakuwa na nguvu katika muda ambao yatapokelewa na mpokea mapendekezo.

Mikataba **kupitia**  
mifumo  
**inayojiendesha**

**26.-**(1) Mkataba ulioingwa kwa njia ya mwiningiliano kati ya mfumo unayojiendesha wenyewe na mtu binafsi au mifumo yenyewe, haitapoteza nguvu ya kisheria kutokana na sababu kuwa hakuna mtu aliyefanya mapitio ya matendo ya kila mmoja wao yaliyotendwa kwa mifumo kuingiliana.

(2) Mfumo unaojiendesha wenyewe utatoa nafasi kwa mtu kurekebisha kosa lolote la kiuingizaji wa taarifa lililofanywa katika mawasiliano ya kielektroniki baina ya mifumo inayointiliana na mhusika wa upande wa pili.

(3) Endapo mtu anafanya kosa la kiuingizaji kwenye mawasiliano ya kielektroniki baina ya mifumo unaojiendesha wenyewe na mhusika wa upande wa pili na mfumo huo

unaoingiliana hautoi nafasi kwa mtu kurekebisha kosa **hilo**, mtu huyo atakuwa na haki ya kuondoa mawasiliano hayo ya kielektroniki ambamo ndani yake amefanya kosa la kiuingizaji, wapo-

- (a) anamtaarifu mhusika wa upande wa pili kuhusiana na kosa hilo haraka iwezekanavyo baada ya kugundua kosa hilo na anakusudia kusitisha mkataba au kurekebisha kosa la kiuingizaji ;
- (b) anachukua hatua madhubuti kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na upande wa pili kurudisha bidhaa au huduma alizopokea kutokana na kutendeka kwa kosa hilo au kuharibu bidhaa au huduma au kurekebisha kosa hilo; na
- (c) hajatumia au kupokea faida yoyote au thamani ya bidhaa au huduma hiyo au kosa la kiuingizaji kutoka kwa mhusika wa upande wa pili.

(4) Mtu ambaye ameshalipia bidhaa au huduma kabla ya kutekeleza haki iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1), atastahili kurudishiwa malipo yake yote ndani ya siku thelathini baada ya kufutwa kwa muamala.

(5) Hakuna kitu chochote katika kifungu hiki kitakachoathiri matumizi ya sheria yoyote inayosimamia masuala yatokanayo na makosa yaliyofanywa wakati wa ufwugwaji au utekelezaji wa aina ya mkataba huo mbali na kosa linalo husiana na uingizaji linatokea katika mazingira ya kifungu kidogo cha (3).

Mnada  
kupitia  
mtandao

**27.** Endapo sheria inahitaji mkataba wa mauzo, utekelezwe kwa njia ya mnada, masharti ya “nyundo kugongwa” yatakuwa yamezingatiwa katika mnada utakaofanyika kupitia mtandao kwa kutumia muda ambao mawasiliano ya kielektroniki yalipokelewa kama kigezo cha ukomo wa muda kama njia ya kumchagua mzabuni wa mwisho.

**SEHEMU YA SITA  
ULINZI KWA MTUMIAJI**

Wajibu wa  
watoa  
huduma kwa  
watumiaji  
wa mtandao

**28-(1)** Mtoa huduma anayeuzza bidhaa au huduma kwa ajili ya mauzo, kukodisha au kwa ajili ya kubadilishana kwa njia ya kielektroniki, atatoa taarifa zifuatazo kwa watumiaji-

- (a) jina kamili, hadi ya kisheria na eneo la biashara;
- (b) maelezo yanayohusu anuwani yake kupatikana kwake zikijumuisha anuani ya makazi, nambari za simu na anuani ya barua pepe;
- (c) maelezo kamili ya bidhaa au huduma zinazotolewa;
- (d) bei ya bidhaa au huduma hiyo;
- (e) taarifa inayohusu malipo yatakayofanywa kwa mujibu wa sheria nyingine; na
- (f) taarifa nyingine yoyote muhimu.

(2) Kabla ya mtumiaji hajatoa maombi yake ya bidhaa au huduma, mtoa huduma atatoa nafasi kwa mtumiaji ya -

- (a) kufanya mapitio ya muamala mzima wa kielektroniki;
- (b) kurekebisha makosa yoyote; na
- (c) kujitoa kwenye muamala huo.

(3) Endapo mtoa huduma anakiuka masharti ya kifungu hiki, mtumiaji anawenza, ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea bidhaa au huduma, kufuta muamala.

Muda kwa  
ajili ya  
kutekeleza  
agizo

**29.-1)** Isipokuwa kama wahusika wamekubaliana vinginevyo, mtoa huduma atatekeleza agizo ndani ya siku thelathini kutokea siku ambayo mtoa huduma amepokea maombi ya bidhaa au huduma.

(2) Endapo mto a huduma anashindwa kutekeleza agizo ndani ya muda uliotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1), mtumiaji anaweza kufuta makubaliano kwa kutoa taarifa ya siku saba.

(3) Endapo mto a huduma anashindwa kutekeleza mkataba kutokana na sababu kuwa bidhaa au huduma zilizoagizwa hazipatikani, mto a huduma, ndani ya siku thelathini, atamtaarifu mtumiaji na mto a huduma atarudisha malipo yoyote ambayo yatakuwa yamefanyika.

Haki ya  
usitishaji

**30.-(1)** Bila ya kuathiri sheria nyingine yoyote, mtumiaji, anaweza ndani ya siku saba au muda mwininge zaidi uliokubalika ndani ya mkataba, baada ya kupokea bidhaa au kukamilika kwa makubaliano na mtumiaji hajapokea faida yoyote kutokana na miamala, huo kufuta makubaliano hayo kwa ajili ya usambazaji wa bidhaa au utolewaji wa huduma.

(2) Endapo mtumiaji anaafuta mkataba chini ya kifungu kidogo cha (1), atalipa gharama zote za moja kwa moja za kurudisha bidhaa.

(3) Endapo mtumiaji amelipia bidhaa au huduma kabla ya kutekeleza haki iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1), atastahili kurudishiwa fedha.

(4) Fedha itakayotolewa chini ya kifungu kidogo cha (3) italipwa ndani ya siku thelathini baada ya tarehe ya kufutwa kwa muamala.

(5) Kifungu hiki hakitatumika kwa miamala ya kielektroniki-

- (a) kwa ajili ya huduma za kifedha;
- (b) kwa njia ya mnada;
- (c) kwa usambazaji wa vyakula, vinywaji au bidhaa nyingine zilizokusudiwea kwa ajili ya matumizi ya kila siku;

- (d) kwa huduma zilizotokana na idhini ya mtumiaji kabla ya kupita kwa muda wa siku saba;
  - (e) iwapo bei ya kusambaza bidhaa au huduma inategemea mfumuko wa bei katika masoko ya fedha na ambayo hayawezi kudhibitiwa na mtumiaji;
  - (f) iwapo bidhaa:
    - (i) zimetengenezwa ili kukidhi matakwa ya mtumiaji;
    - (ii) zimetengenezwa maalum kwa ajili maalum;
    - (iii) kutokana na hali yake, haziwezi kurudishwa; au
    - (iv) zina uwezekano wa kuharibika au kupitwa na muda wa matumizi haraka;
  - (g) iwapo rekodi za kusikiliza au za video au programu za kompyuta zilipakuliwa au kuondolewa lakiri na mtumiaji;
  - (h) kwa ajili ya uuzaaji wa magazeti, makala, majarida na vitabu;
  - (i) kwa ajili ya kutolewa kwa huduma za michezo ya kubahatisha au bahati nasibu;
  - (j) kwa ajili ya michezo ya kubahatisha inayofanyika kwa kupitia mtandao;
  - (k) kwa ajili ya kutolea huduma za malazi, usafiri na chakula; na
  - (l) kwa kadri ambavyo Waziri anaweza kwa tangazo litakalochapishwa kwenye *Gazeti* la Serikali, kuanzisha miamala mingine yoyote.
- (6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, “gharama za moja kwa moja” maana yake ni gharama zilizoingiwa na zinajumuisha gharama za usafiri au kutumia wakati wa kurudisha bidhaa au huduma, isipokuwa haitajumuisha gharama zozote za upakiaji au usambazaji.

Taarifa zitakazo  
tolewa katika  
mawasiliano ya  
kielektroniki

**31.-**(1) Mtu anayeuzza bidhaa au huduma za mawasiliano ya kielektroniki atampatia mlengwa –

- (a) utambulisho wa chanzo cha mawasiliano na maelezo kuhusiana na anuwani yake;
- (b) chombo halali cha utekelezaji ambacho kitatoa nafasi ya mtu kuamua kutokuendelea kupokea mawasiliano katika siku za mbele; na
- (c) maelezo kuhusiana na chanzo ambacho kutoka kweke chanzo cha mawasiliano kilipata taarifa binafsi za mlengwa.

Bidhaa, huduma  
au mawasiliano  
ambayo  
hayajaombwa

**32.-**(1) Mtu hatatuma mawasiliano ya kibashara yanayphusu bidhaa au huduma ambazo hazijaombwa na mlengwa, isipokuwa kama-

- (a) mtumiaji anaridhia mawasiliano hayo;
- (b) mwanzoni mwa mawasiliano, mawasiliano hayo yanaweka wazi utambulisho wa mtumaji na madhumuni ya mawasiliano; au
- (c) mawasiliano hayo yanaweka utaratibu wa kukataa mawasiliano hayo siku zijazo.

(2) Masharti ya mtu kuridhia ama kutokuridhia yatachukuliwa kuwa yametimizwa iwapo-

- (a) anuwani ya mlengwa wa mawasiliano na taarifa nyingine binafsi ambayo ilikusanywa na mtuma taarifa wakati wa mauzo au majadiliano kwa ajili ya mauzo;
- (b) mtuma taarifa anatuma matangazo ya biashara yanayohusiana bidhaa au huduma zinazofanana kwa mlengwa;
- (c) mto taarifa ametoa nafasi kwa mlengwa fursa ya kujitoa na kufanya hivyo; na

(d) fursa ya kujitoa imetolewa na mtoa taarifa kwenda kwa mlengwa kwa kila ujumbe utakaotumwa.

(3) Mtuma taarifa atayayekiuka masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na atawajibika, pale atakapotiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

### SEHEMU YA SABA WATOA HUDUMA ZA KRAIPTOGRAFIA NA UIDHINISHAJI

Huduma za kraiptografia na uidhinishaji

**33.** Waziri anaweza, kwa taarifa itakayochapishwa kwenye *Gazeti la Serikali*, kuteua taasisi ya kiserikali chini ya Wizara yenyeye dhamana na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kuwa mdhibiti wa Huduma za Kraiptografia na Uidhinishaji.

Majukumu ya mdhibiti

**34.** Majukumu ya mdhibiti huyo yatakuwa ni-

- (a) kutoa leseni na kusimamia huduma za kraiptografia na uidhinishaji;
- (b) kuainisha viwango vya kiusalama vya kraiptografia na saini za za kielektroniki;
- (c) kuamua viwango vitakavyozingatiwa na mamlaka za uidhinishaji;
- (d) kuweka na kutunza rejestra ya watoa huduma wa huduma za kraiptografia na uidhinishaji; na
- (e) kufanya vitu vingine vyovoyote ambavyo ni muhimu kwa utekelezaji wa masharti ya Sehemu hii.

Maombi ya usajili

**35.** (1) Mtu anayekusudia kutoa huduma za kraiptografia au uidhinishaji atawasilisha maombi yake kwa mdhibiti .

(2) Maombi yaliyofanywa chini ya kifungu kidogo cha (1) yatakuwa na maelezo yafuatayo:

- (a) jina na mawasiliano yake, ikijumuisha **anuwani** ya makazi, simu na barua pepe;
- (b) maelezo yanayohusu aina ya huduma itakayotolewa;
- (c) maelezo ya madhumuni ya huduma itakayotolewa;
- (d) maelezo yanayohusu teknolojia itakayotumika katika utowaji wa huduma hiyo; na
- (e) maelezo mengine yoyote kwa kadri itakavyoelekezwa na msimamizi.

Katazo la kutoa  
huduma za  
kraiptografia au  
uidhinishaji

**36.**-(1) Mtu hatatoa huduma za kraiptografia au uidhinishaji bila ya kuwa na leseni.

(2) Mtu atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na iwapo atatiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano au vyote kwa pamoja.

#### SEHEMU YA NANE MASHARTI YA JUMLA

Mamlaka ya  
kutunga kanuni

**37.** Waziri anaweza kutunga kanuni kwa jumla zinazohusu jambo lolote ambalo linatakiwa kuainishwa na Sheria hii au ambalo ni la umuhimu kwa ajili ya utekelezaji **bora** wa masharti ya Sheria hii.

#### SEHEMU YA TISA MASHARTI YATONANAYO PART IX CONSEQUENTIAL AMENDMENTS

*(a) Amendment of the Law of Contract Act, Cap. 345*

Construction  
Cap.345

**38.** This Part shall be read as one with the Law of Contract Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Amendment of  
section 10

**39.** The principal Act is amended in section 10 by inserting the words “or in electronic form” immediately after the words “in writing” appearing in the proviso of that section.

Amendment of  
section 25

**40.** The principal Act is amended in section 25, by –  
the following:

“Agreement without consideration is void”

- (c) inserting the words “in electronic form” immediately after the word “writing” appearing in paragraph (a);
- (d) inserting the words “or electronic form” immediately after the word “writing” appearing in paragraph (c);

*(b) Amendment of the Law of Evidence Act, Cap.6*

Construction  
Cap. 6

**41.** This Part shall be read as one with the Law of Evidence Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Amendment of  
section 3

**42.** The principal Act is amended in section 3 by deleting the definition of the term “document” and substituting for it with the following:

“document” means any writing, handwriting, typewriting, printing, Photostat, photography, computer data and every recording upon any tangible thing, any form of communication or representation including in electronic form, by letters, figures, marks or symbols or more than one of these means, which may be used for the purpose of recording any matter provided that recording is reasonably permanent and readable;.

Amendment of  
section 19

**43.** Section 19 of the principal Act is amended by inserting the word “electronic” immediately after the word “oral”;

Amendment of  
section 34

**44.** Section 34 of the principal Act is amended by inserting the word “electronic” immediately after the word “written”;

Amendment of  
section 34B

**45.** Section 34B of the principal Act is amended by inserting the words “or electronic” between the words “written” and “statements” wherever they appear in that section.

Addition of  
section 64A

**46.** The principal Act is amended by adding a new section 64A as follows:

“Admisibi  
lity of  
electronic  
evidence

**64A.-**(1) In any proceedings, electronic evidence shall be admissible.

(2) The admissibility and weight of electronic evidence shall be determined in the manner prescribed under section 18 of the Electronic Transaction Act, 2015.

(3) For the purpose of this section, “electronic evidence” means any data or information stored in electronic form or electronic media or retrieved from a computer system, which can be presented as evidence.”

*(c) Amendment of the Records and Archives Management Act, Cap.309*

Construction  
Cap.309

**47.** This Part shall be read as one with the Records and Archives Management Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Amendment of  
section 2

**48.** The principal Act is amended in section 2 by inserting the words “or electronic” immediately after the word “recorded” appearing in the definition of the term “record”.

*(d) Amendment of the Banking and Financial Institutions Act, Cap.342*

Construction  
Cap.342

**49.** This Part shall be read as one with the Banking and Financial Institutions Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Amendment of  
section 8

**50.** The principal Act is amended in section 8 by inserting the words “or in electronic form” between the words “writing” and “and”, appearing in subsection (1).

Imepitishwa na Bunge tarehe 1 Aprili, 2015.

THOMAS D. KASHILILAH

Katibu wa Bunge